

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia



# MATOKEO CHANYA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

JULY 2025

3

**Mageuzi Ya Kihistoria Katika Elimu, Sayansi Na Teknolojia**




12

**Eastrip Yaleta Mapinduzi Elimu Ya Ufundi Tanzania**





6

**Uboreshaji Wa Miundombinu Ya Elimu Msingi, Sekondari Na Ualimu**



Kazi Iendelee

www.moe.go.tz

## BODI YA WAHARIRI

Sylvia Lupembe
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta
Dionice Lukweme
Fradius Mugoa



**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533



**Jarida hili linatolewa na:**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# Tahariri: Mageuzi ya Kihistoria Katika Elimu, Sayansi na Teknolojia



Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali ya Tanzania Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio na kuanza utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, inayolenga kuzalisha nguvu kazi mathubuti yenye maarifa, stadi stahiki na ujuzi.

Serikali imeongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa makundi yote ya jamii kupitia sera ya utoaji wa elimu bila malipo, inayo jumuisha elimu ya awali hadi sekondari ya juu. Aidha imepiga hatua kubwa kwa kuongeza fursa za mikopo ya elimu ya juu, hatua hii imewawezesha vijana wengi kufikia ndoto zao za kielimu.

Kwa kutambua kuwa walimu ni nguzo muhimu katika maendeleo ya elimu nchini, Serikali imeongeza fursa za ajira, kuboresha maslahi ya walimu ili kuongeza motisha kazini na kuwezesha mafunzo endelevu ya walimu kazini kuwajengea ujuzi mpya



na mbinu za kisasa za ufundishaji.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa muongozo thabiti katika kuimarisha sekta ya elimu. Inaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Wizara za Kisekta, Wadau wa Maendeleo, wadau wa elimu na jamii kwa ujumla, tunatambua mchango wenu umetuwezesha kufikia malengo katika utoaji wa elimu bora nchini.



# Elimu na Ujuzi Kujenga Taifa Lenye Uchumi Imara








Serikali ya Awamu ya Sita imeandika historia kwa kufanya mapitio na kuanza utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023. Hatua hii ya kimkakati inalenga kubadilisha mfumo wa elimu nchini kuwa wa kisasa, jumuishi na wenye ufanisi zaidi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Sera hiyo, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alieleza kuwa lengo la mabadiliko ya sera ni kuwaandaa vijana kwa kuwapatia wahitimu nyenzo zitakazowawezesha kushindana kikanda na kimataifa, ili waweze kunufaika kiuchumi kupitia rasilimali za taifa.

Mhe. Dkt. Samia alisisitiza kuwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI, kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera na Mitaala mipya ya Elimu, ili ilete matokeo yaliyokusudiwa.

Naye, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango alisisitiza kuwa kuyakabili mabadiliko ya teknolojia Sera ya elimu inapaswa kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi wa kumudu teknolojia mbalimbali na ushindani wa kibishara duniani.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alifafanua kuwa katika sera hiyo, muda wa elimu ya lazima umeongezwa kutoka miaka saba hadi miaka 10, hatua inayojumuisha elimu ya msingi ya miaka sita, na sekondari ya chini ya miaka minne.



# Serikali Yawarejesha Wanafunzi Zaidi 22,000 Shuleni



**22,844**

Katika hatua ya kihistoria ya kuimarisha usawa wa fursa za elimu, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuwarejesha shuleni jumla ya wanafunzi **22,844** waliokuwa wamekatiza masomo kwa sababu mbalimbali, ikiwemo ujauzito, ndoa za utotoni, na changamoto za kifamilia.

Hatua hii ni utekelezaji wa Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 2021, uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ukiruhusu wanafunzi waliokatiza masomo kurejea shuleni kwa mfumo rasmi na usio rasmi

Wanafunzi **5,142** wamejiunga tena kupitia mfumo rasmi wa elimu

Wanafunzi **17,702** wakirejea kupitia mfumo usio rasmi kama vile Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Mpango huu umepongezwa na wadau wa elimu, mashirika ya kijamii, na wazazi, wakisema ni hatua ya kuondoa unyanyapaa na kuimarisha haki ya elimu kwa wasichana na wavulana waliokumbwa na changamoto za maisha.

**Aidha, Serikali inatekeleza mikakati ya kutoa msaada wa kisaikolojia, huduma za malezi ya watoto, na ufadhili wa elimu kwa wanafunzi waliorejea shuleni.**

**Wanafunzi waliorejea wamesema wanajisikia kuthaminiwa na kupewa nafasi ya pili ya kujenga maisha yao**

*"Nashukuru kwa kurudi shuleni, natamani kuwa muuguzi na kusaidia wasichana wengine wasikate tamaa."*

**Mwanafunzi, kidato cha pili - Morogoro.**



# Uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu Msingi, Sekondari na Ualimu



Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali imejenga:

**Madarasa**: 334
- Msingi: 263
- Sekondari: 71

**Matundu ya vyoo**: 4,207
- Msingi: 3,799
- Sekondari: 408

**Mabweni**: 334 katika shule za sekondari

**Nyumba za walimu**: 63 katika shule za msingi

**Mabwalo**: 7

**Matenki ya kuhifadhia maji**: 140, katika shule za msingi **139**

**Ukarabati vituo vya ualimu (TRCs)**: 85

Aidha, serikali imefadhili wanachuo **787**.

Wanaume **358**

Wanawake **429**

***kusoma Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum***

Sambamba na hayo, Serikali imenunua na kusambaza

- vitimwendo **120**
- kompyuta mpakato **35**
- vinasa sauti vya kidigiti **48**
- vishikwambi **45**

kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 120 katika halmashauri ambazo zilibainika kuwa na wanafunzi wengi wenye ulemavu wa viungo.

Vilevile, jumla ya wanafunzi **691** wamepatiwa vifaa mbalimbali ikiwemo kompyuta mpakato, vitimwendo na vinasa sauti.

Aidha katika kuongeza fursa za elimu ya amali, Serikali imewezesha ujenzi wa shule mpya **103** za sekondari za amali. Kati ya shule hizo, **29** ni za amali za kihandisi na **74** ni za amali zisizo za kihandisi, ambapo kukamilika kwake kutaongeza idadi ya shule za amali kutoka tisa (**9**) hadi **112**.





# BOOST Yaweka Msingi Imara ya Miundombinu Elimu ya Awali na Msingi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza Mradi wa Kuimarisha na Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara kupitia Mkopo wa Masharti nafuu wa Benki ya Dunia. Mradi huu wa miaka 5 ulianza kutekelezwa Disemba 2021 hadi Disemba 2026, ukigharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni 500.

### Madarasa 7,230 Yamejengwa

Program hii imewezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa **7,230** katika Halmashauri mbalimbali nchini, madarasa **3,880** yamejengwa katika shule mpya **302** na madarasa **3,350** yamejengwa shule zilizokuwa na uhaba. Aidha, imewezesha ujenzi wa matundu ya vyoo **11,295**, majengo ya utawala **302** na nyumba za walimu **40**.

### Mafunzo ya walimu yameimarishwa

Serikali imewajengea uwezo wakufunzi 189 wa Vyuo vya Ualimu 16 vinavyoandaa walimu wa Elimu ya Awali ngazi ya Astashahada wamejengewa uwezo na Wathibiti ubora wa Shule 480 kutoka Halmashauri zote wa kufuatilia utolewaji wa elimu ya awali.

### 89.6% Kiwango cha Uandikishaji

Utekelezaji wa Programu hii umechagiza uandikishaji wa Elimu ya Awali uliongezeka kwa zaidi ya 1.6%, iliyowekwa kila mwaka na kufikia asilimia kati ya 5% na 9%. Hadi kufikia 2024/25 uwiano wa uandiskishaji umefikia asilimia 89.62%

### Programu ya Shule Salama

Mpango wa Shule salama unawapa uwezo maelfu ya maafisa na viongozi wa elimu, wakiwemo washauri wa walimu 3,800 na waratibu wa kata 680, ili kuhakikisha mazingira salama ya kujifunzia.

### Walimu Wakuu 18,798 Shule za Msingi wapata mafunzo

Mafunzo kuhusu usimamizi bora wa Shule, uwezo juu ya masuala ya Utawala bora. Maafisa Elimu Mkoa, Maafisa Elimu Msingi, Wakaguzi wa Hesabu wa ndani wa Halmashauri na Maafisa Mipango wa Halmashauri zote.

### Walimu 49,300 Wapata Mafunzo

Walimu wapatao 49,300 wamepatiwa mafunzo mbalimbali endelevu Kazini (MEWAKA) kuhusu utambuzi wa vifaa vya TEHAMA. Hii ni pamoja na kuweka vifaa vya TEHAMA katika vituo vya Walimu 400 kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji






BOOST
Primary Student
Learning Program



# SEQUIP Yaboresha Miundombinu ya Sekondari

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, inatekeleza **Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP),** unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 500. Mradi huu umeleta mafanikio makubwa katika miundombinu ya shule za sekondari nchini.



## Ujenzi wa Madarasa na Majengo Mengine

| Vyumba vya madarasa | mabweni ya wanafunzi | matundu ya vyoo | maabara za sayansi | nyumba za walimu |
|---|---|---|---|---|
| 1,499 | 625 | 165 | 132 | 45 |

## Shule za Amali Zapewa Kipaumebele

Kati ya shule za sekondari za Kata **231** zinazojengwa kupitia Mradi huu, shule 23 tayari zimekamilika, huku shule nyingine **208** zikiwa katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Vile vile ujenzi Shule za sekondari za Amali **103** kupitia mpango huu, nazo zimepewa kipaumbele, zikihusisha shule **29** za kihandisi na shule **74** zisizo za kihandisi.





## Uwezeshaji Masomo ya Sayansi kwa Wasichana

Mafanikio ya SEQUIP yameonyesha ubora wake kupitia ujenzi wa Shule ya Sekondari ya **Dkt. Samia Suluhu** mkoani Ruvuma, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **1,200**. Shule hii ni sehemu ya mpango wa shule za sayansi za wasichana za mikoa yote **26** zinazojengwa kupitia mradi huu.

# Fursa za Elimu ya Ufundi Zaongezeka: VETA kila Wilaya

### Shule 103 Mpya, Sekondari za Amali Zajengwa

Katika kuongeza fursa za elimu ya amali, Serikali imewezesha ujenzi wa shule mpya **103** za sekondari za amali.

**29** Shule za amali za kihandisi

**74** Shule za amali zisizo za kihandisi

ambapo kukamilika kwake kutaongeza idadi ya shule za amali kutoka tisa **(9)** hadi **112**.

Udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi umeongezeka hadi kufikia

**199,118** (**2024/25**) Ikilinganishwa na **161,750** (**2021/22**)

Ikiwa ni ongezeko la wanafunzi **337,368** = **23%**

Mafanikio hayo yanatokana na kuongezeka kwa vyuo vya elimu ya ufundi kutoka vyuo **441** mwaka 2021/22 hadi kufikia vyuo **512** mwaka 2024/25.

Mwaka 2025 wanafunzi 11,232 walidahiliwa katika vyuo vya VETA. Vyuo hivyo vimeongezeka hadi kufikia 905 mwaka 2025 kutoka vyuo 810 mwaka 2022. Aidha wanafunzi 391 wamedahiliwa katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro.



Serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo 64 vya wilaya, ujenzi wa vyuo 63 umefikia wastani wa asilimia 45, chuo cha wilaya ya Chamwino asilimia 88 na cha mkoa wa Songwe kimefikia asilimia 40. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya nyongeza katika vyuo 10 vya mafunzo ya ufundi stadi umefikia wastani wa asilimia 82.

Serikali imefadhili mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,724 katika kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo cha Ufundi Arusha, na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Aidha, imewezesha huduma ya chakula kwa wanafunzi 17,411 katika vyuo husika.





# EASTRIP Yaleta Mapinduzi Elimu ya Ufundi Tanzania



**Mradi wa Dola za Kimarekani Milioni 75**

Tanzania imefungua ukurasa mpya wa maendeleo kwa sekta ya elimu ya ufundi kupitia **Mradi wa Kujenga Ujuzi na Mtangamano wa Kikanda wa Afrika Mashariki *(EASTRIP)***, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa lengo la kuinua ubora na upatikanaji wa elimu ya ufundi katika vituo maalum vya umahiri nchini Tanzania, Kenya na Ethiopia



Serikali imepokea Dola za Kimarekani ***milioni 75*** kuboresha miundombinu, mitaala, na mafunzo ya walimu ikiwa ni sehemu ya kuimarisha ushirikiano na sekta za viwanda katika vyuo vya **ATC, NIT, DIT** pamoja na **DIT** kampasi ya **Mwanza**.

Chuo cha NIT imefadhili mafunzo walimu **17** katika nchi mbalimbali duniani, na kutoa ufadhili kwa wanafunzi **44** wa kike katika fani za usafiri wa anga na operesheni za usafirishaji.

Kwa upande wa uchakataji wa ngozi, DIT Mwanza imeongeza idadi ya wanafunzi kutoka **81** hadi **791** kwa mwaka, na kusaini mikataba na viwanda kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Aidha Chuo cha ATC kimejipatia sifa kutokana na ujenzi wa kituo cha mafunzo ya nishati jadidifu katika kampasi ya Kikuletwa.

Kwa upande wa uchakataji wa ngozi, DIT Mwanza imeongeza idadi ya wanafunzi kutoka **81** hadi **791** kwa mwaka, na kusaini mikataba na viwanda kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Aidha Chuo cha ATC kimejipatia sifa kutokana na ujenzi wa kituo cha mafunzo ya nishati jadidifu katika kampasi ya Kikuletwa.

Mradi huu pia umeongeza ushirikiano wa kikanda kwa kuhimiza ubadilishanaji wa sera, utafiti wa pamoja, na mafunzo ya walimu katika nchi washirika.



# Serikali Yazindua Miongozo Ya Kidijitali Kuimarisha Elimu Nchini



## Mwongozo wa Matumizi ya Akili Mnemba

Katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknlojia imechukua hatua ya kihistoria katika kuinua ubora wa elimu kwa kutumia teknolojia, baada ya kuzindua rasmi **Mwongozo wa Taifa wa Matumizi ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence)** katika Elimu.

Mwongozo huo unatoa miongozo ya kielimu kuhusu matumizi salama na madhubuti ya teknolojia ya akili mnemba, kuanzia upangaji wa masomo, upimaji wa maendeleo, mpaka usimamizi wa taarifa za shule. Unalenga pia kuhimiza utafiti na bunifu zinazotumia Akili Unde, hasa katika masomo ya STEM.

Sambamba na kugawa vishkwambi zaidi ya **285,000** kwa walimu na wakufunzi nchi nzima vikiwa vimeunganishwa na mifumo ya TEHAMA yenye maudhui ya kitaaluma, mitaala ya kidijitali, na programu maalum za ufundishaji.

Aidha, kuongeza ufanisi katika ufundishaji, kurahisisha ujifunzaji wa wanafunzi, na kufuatilia maendeleo yao kitaaluma kupitia mifumo ya kidijitali. Vishkwambi hivyo vimegawiwa kwa walimu wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na taasisi za elimu ya juu.



# Tuzo ya Mwalimu Nyerere Yaleta Mapinduzi ya Fasihi Tanzania: Waandishi Wazidi Kung'ara




Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ni mpango wa kitaifa ulioanzishwa na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ili kuenzi mchango wa Hayati Mwalimu Julius Nyerere katika elimu na fasihi. Tuzo hii inalenga kuhamasisha ubunifu wa waandishi wa Kiswahili, kukuza usomaji, na kurudisha heshima ya fasihi kama nyenzo ya maarifa na mabadiliko ya kijamii. Kupitia jukwaa hili, waandishi wanapata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao kwa kuchapishwa na kusambaza kazi zao nchini.

## Washindi wa Tuzo

**1** — **Sh. milioni 10** (cheti cha heshima na miswada yao kuchapishwa na kusambazwa mashuleni na kwenye maktaba)

**2** — **Sh. milioni 7**

**3** — **Sh. milioni 5**

Mwaka
**2025**

## Miswada 282 Imepokelewa

tuzo hii imeendelea kuonyesha ukuaji mkubwa kwa kupokea jumla ya miswada **282** kutoka kwa waandishi wa ndani ya nchi

| | |
|---|---|
| **114** kazi za ushairi | **46** kazi za riwaya |
| **77** hadithi za watoto | **45** tamthiliya |



**Nakala 148,000 Zachapishwa**

Kupitia mashindano hayo nakala za **vitabu 148,000** zimechapishwa na kusambazwa katika shule za sekondari na msingi

**70,000** Riwaya

**70,000** Ushairi

**8,000** Hadithi za Watoto

**Nakala zilizochapwa 2024/25 vs 2021/22**

| 2024/25 | 2021/22 |
| --- | --- |
| Serikali imechapa na kusambaza nakala **16,795,403** za vitabu vya kiada ngazi ya elimu ya awali na msingi. | Serikali ilichapa na kusambaza nakala **12,197,434** za vitabu vya kiada ngazi ya elimu ya awali na msingi. |

Akizungumzia kuhusu mashindano ya tuzo hizo, Mhadhiri Mwandishi wa Vitabu na Mchoraji maarufu kutoka Chuo Kikuu cha Sultan Qaboos, Oman Profesa Ibrahim Noor Sharif, alisisitiza nafasi ya Akili Mnemba (AI) katika kusaidia waandishi wa Kiswahili kufikia hadhira ya kimataifa, hatua inayoweza kuitangaza Tanzania kama kitovu cha fasihi bunifu Afrika.

Aidha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kuratibu Mashindano ya Uandishi wa Insha za EAC na SADC zinazolenga kuchochea ubunifu na utafiti katika masuala ya kikanda pamoja na kuzitambua talanta na kukuza ujuzi kwa vijana ambao umechagiza ushirikiano kati ya nchi wanachama wanaoshiriki katika mashindano hayo.



# Fursa za Mikopo Elimu ya Juu Zaimarika





## Bajeti ya Mikopo Elimu ya Juu Yapaa na Kufikia Sh. bilioni 787.4

Bil 570

Bil 787.4




2021/22

2024/25

Katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu hadi kufikia Sh. bilioni 787.4 kutoka Sh. bilioni 570 zilizotolewa mwaka 2021/22.

Vilevile, imetoa mikopo kwa ngazi ya elimu ya stashahada (Diploma) kwa kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 19.95 kwa wanafunzi 7,534 wa fani za sayansi na ufundi kwa mwaka wa fedha 2024/25 ikiwa ni ongezeko la asilimia 177.6 ikilinganishwa na wanafunzi 2,714 waliopata mikopo hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

## SAMIA Skolashipu

Kupitia SAMIA Skolashipu Serikali imetoa ufadhili wenye thamani ya **Sh. bilioni 7.29** kwa wanafunzi **646** wa mwaka wa kwanza na wanafunzi wanaoendelea (shahada wa kwanza **674** na ngazi ya umahiri 80) wenye ufaulu uliojipambanua katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

## SAMIA Extended Skolashipu

Sambamba na ufadhili huo, Serikali kwa mara ya kwanza imeanza kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma shahada za juu katika sayansi na teknolojia ya nyuklia nje ya nchi kupitia **SAMIA Extended Skolashipu** ambapo wanafunzi watano (**5**) wamenufaika.

Aidha, Serikali imetangaza ufadhili wa masomo kwa mwaka wa 2025/26 kupitia programu ya **SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+ (SSE-DS/AI+)**, kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza na Umahiri. Ufadhili huu unalenga wanafunzi watakaojiendeleza kitaaluma katika fani za Data Science, Artificial Intelligence, Cybersecurity, Machine Learning na Allied Science.

# HEET Yaweka Historia Mpya Elimu ya Juu



**Mradi wa Shilingi bilioni 972**

Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuinua ubora wa elimu ya Juu naolenga kutoa wahitimu wenye maarifa na ujuzi stahiki unaokidhi soko la ajira kitaifa na kimataifa sambamba na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Kutokana na dhamira hiyo imekuwa mstari wa mbele kuwekeza katika miradi ya kimkakati inayolenga kuinua ubora wa elimu, miundombinu, na rasilimali watu. Mojawapo ya jitihada hizi ni utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), unaolenga kuleta mageuzi chanya katika sekta ya elimu ya juu kwa kuendana na mahitaji ya uchumi wa kisasa.

Mradi huu wa Shilingi bilioni 972 unafadhiliwa kwa ushirikiano na Benki ya Dunia, unalenga kuimarisha taasisi za elimu ya juu kupitia maboresho ya mitaala, ujenzi wa miundombinu, kuongeza matumizi ya teknolojia na mafunzo kwa wahadhiri.

Katika kuleta mapinduzi ya elimu ya juu, Serikali inaendelea na ujenzi wa Kampasi mpya 16 katika mikoa iliyopo pembezoni ikiwemo Katavi, Simiyu, Njombe, Lindi, Rukwa, Songwe na Geita ili kusogeza fursa za elimu karibu kwa wananchi na kuchochea maendeleo.

Akizungumza katika hafla ya kuweka jiwe la msingi la Kampasi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) mkoani Rukwa, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alisisitiza umuhimu wa kupeleka elimu karibu na wananchi.

Pamaoja na ujenzi wa miundombinu, imetoa fursa za mafunzo kwa wahadiri 559 kutoka wa vyuo vikuu vya umma na 27 binafsi katika programu za umahiri na Uzamivu.

Aidha, kupitia Mradi wa HEET, jumla ya Mitaala 563 ya taasisi za Elimu ya Juu imehuishwa, kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira na fursa za mikopo Elimu ya Juu maendeleo ya kiuchumi.



# Bilioni 25.7 Kuimarisha Ubunifu na Tafiti Bunifu

## COSTECH yapatiwa Sh. bilioni 25.7

Serikali ya Awamu ya Sita imepiga hatua kubwa katika kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kuwekeza kiasi cha **Sh. bilioni 25.7** kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia **(COSTECH)** kwa ajili ya kufadhili tafiti bunifu, kuimarisha miundombinu ya ubunifu, na kuchochea uanzishaji wa biashara mpya zenye msingi wa kiteknolojia.

## Tafiti Zafadhiliwa, Vituo Bunifu Vyaimarishwa

Kwa mujibu wa taarifa kutoka COSTECH, fedha hizo zimetumika kufadhili tafiti zaidi ya **50** zinazogusa sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, afya, nishati jadidifu, elimu, na TEHAMA. Pia, zaidi ya **vituo 111 vya ubunifu** vimeimarishwa katika vyuo vikuu, taasisi za elimu ya juu, na mabaraza ya ujasiriamali wa vijana nchini.

## Kampuni 70 Mpya za Vijana Zaundwa

Matokeo ya uwekezaji huu yameonekana moja kwa moja katika uundaji wa kampuni **70** mpya zilizoanzishwa na vijana waliopata msaada wa kifedha na kiufundi kupitia COSTECH. Kampuni hizo zinajihusisha na uzalishaji wa bidhaa za teknolojia, mifumo ya kidijitali, na huduma za ubunifu zinazotatua changamoto halisi za jamii.





Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambao unasisitiza uboreshaji wa mazingira ya utafiti na uanzishwaji wa kampuni bunifu zinazoweza kuhimili ushintdani wa kimataifa.

# Serikali Yafanya Mapinduzi ya Elimu Maalum: Miongozo Mpya Kuhakikisha Usawa, Ushirikishwaji na Elimu Kwa Wote

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya juhudi kubwa kuboresha elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu.

Kupitia Kitengo cha Elimu Maalum, wizara imetoa miongozo mbalimbali inayolenga kuhakikisha ushirikishwaji wa watoto wote katika mfumo wa elimu bila ubaguzi. Hatua hizi zimeongeza upatikanaji wa huduma stahiki, kuimarisha mazingira ya kujifunzia, na kutoa mafunzo kwa walimu ili waweze kuhudumia wanafunzi kwa ufanisi zaidi.

## Mwongozo wa Kitaifa wa Ubainishaji na Upimaji wa Watoto Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu ya Kielimu

Mwongozo huu unaolenga kusaidia walimu na wataalamu kubaini mapema mahitaji maalum ya wanafunzi ili waweze kusaidiwa ipasavyo. Mwongozo huu ni msingi wa utoaji wa huduma sahihi kwa kila mtoto kulingana na changamoto zake za kielimu.

## Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu

Mwongozo huu unawawezesha walimu kufanya tathmini ya mazingira ya nyumbani ya mwanafunzi ili kubaini changamoto zinazoweza kuathiri ujifunzaji wake. Mwongozo huu unalenga kuimarisha ushirikiano kati ya shule na familia katika kusaidia maendeleo ya mwanafunzi.

## Mwongozo wa Shule ya Nyumbani kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuhakikisha watoto ambao hawawezi kufika shuleni kwa sababu za kiafya au mazingira wanapata elimu wakiwa nyumbani. Hii ni hatua ya kipekee ya kuhakikisha hakuna mtoto anayekosa haki ya msingi ya kupata elimu.

## Mwongozo wa Uendeshaji wa Elimu Maalum na Jumuishi

Mwongozo huu unatoa mwelekeo wa kitaifa kuhusu namna ya kuendesha elimu inayojumuisha watoto wote bila kujali hali zao. Mwongozo huu unahimiza ushirikiano kati ya serikali, familia, na wadau wa elimu katika kuhakikisha mazingira rafiki kwa ujifunzaji wa watoto wenye mahitaji maalum.

Jitihada hizi zinaonyesha dhamira ya dhati ya serikali ambapo idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi imeongezeka kutoka **66,083** mwaka 2020 hadi **94,618** mwaka 2024, Sekondari wanafunzi **10,325** mwaka 2020 hadi **25,950** na vyuo vikuu kutoka wanafunzi **60** mwaka 2020 hadi **760** mwaka 2024.


20




Kiswahili
Kitabu cha Mwanafunzi
Darasa la Tatu


a e i o u
ba be bi bo
da de di do
ka ke ki ko



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

@wizarayaelimutanzania